**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KAKONKO**

SHULE YA SEKONDARI KAKONKO
BOYS,
S.L.P 03,
**KAKONKO**

Mzazi/Mlezi wa .........................................................

TAREHE ............................................

YAH: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WAVULANA KAKONKO, WILAYA YA KAKONKO MKOA WA KIGOMA 2026.**

## 1.0 UTANGULIZI.

Nafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza mwaka 2026 katika Shule ya Sekondari ya Wavulana Kakonko. Shule hii ni shule ya bweni na ipo katika kijijini Kasanda, Wilaya ya Kakonko, katika Mkoa wa Kigoma, na ipo umbali wa kilometa 7 kutoka kwenye kitovu cha Kijiji cha Kasanda. Usafiri wa bodaboda kutokea kituo cha mabasi cha Kasanda ni shilingi 5000/=. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 13/01/2026, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe13/01/2026

## 2.0. MAVAZI

### 2.1. SARE ZA SHULE

a) Suruali mbili rangi ya kijivu iliyokolezwa (darkgrey) zenye marinda mawili kushoto na kulia na turnup chini(inchi $1^{1}/_{2}$) na upana wa chini inchi 16,

b) Nguo za kushindia (Shambadress) suruali mbili ya rangi nyeusi zenye marinda mawili kushoto na kulia na turnup chini(inchi $1^{1}/_{2}$) upana wa chini inchi 16,

**N: B** kutokana na changamoto ya kukosea rangi na vipimo zitapatikana shuleni kwa bei nafuu ya shilingi elfu17, 000/= kila suruali,

c) Shati mbili nyeupe zenye mikono mifupi zisizo na mapambo yoyote wala zisibane,

d) Soksi nyeusi jozi mbili,

e) Viatu pea mbili vyeusi vya ngozi vinavyofunika miguu vyenye Kamba na visigino vifupi,

f). T-shirt za shule mbili za rangi ya bluu ya kukoleza (bluu) zenye kola nyeusi na Nembo ya shule zitapatikana shuleni kwa bei nafuu kwa shilingi 15, 000/= kila T-shirt,

g) Sweta rangi ya kijivu iliyokolea itapatikana shuleni kwa Tsh 15,000/=,

h) Kanda mbili kwa ajili ya kuogea na viatu vya wazi kwa ajili ya kuvaa baada ya mda wa masomo,

I) Vesti mbili nyeupe.

N:B Nguo nyingine zozote mbali na sare za shule zilizotajwa hapo juu **HAZIRUHUSIWI**.

### 2.2. SARE ZA MICHEZO

Sare za michezo Kwa shule hii ni kwa wote:

a) Raba nyeusi moja ya michezo kwa wanafunzi wote,

b) Kaptula na T-shirt rangi nyeusi jozi mbili,

c) Track suit kwa wanafunzi wote rangi ya light bluu yenye michirizi myeupe.

## 3.0 MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANATAKIWA KUJA NAYO SHULENI-

### 3.1. VIFAA VYA MASOMO.

i. Madaftari makubwa10 (counterbook quire 3 au 4 kwa ajili ya kuandikia matini (notes) za masomo,
ii. Mkebe wa Hisabati(Mathematical set),
iii. Rula, kalamu na penseli kwa wanafunzi wote,
iv. Graph pad 2,
v. Kamusi ya kingereza (English to English),
vi. Rim1A4 “double A”.

### 3.2. VIFAA VYA USAFI.

i. Aje na mfagio ( hard broom, floor squeezer),
ii. Ndoo mbili za lita kumi,
iii. Beseni la kufulia,
iv. Fyekeo,
v. Jembe.

### 3.3 MALAZI

i. Mwanafunzi aje na godoro futi $2^1/_2$ x 6,
ii. Aje na Mashuka mawili ya rangi ya bluu bahari,
iii. Aje na chandarua rangi ya bluu bahari,
iv. Blanketi nzito.

**3.4 MAHITAJI MENGINE MUHIMU**

i. Mchango wa BIMA YA AFYA CHF Tsh 5000/- au kama ana BIMA YA AFYA, aje nayo,
ii. Kila mwanafunzi aje na Tranka imara la kutunzia vifaa vyake lenye kufuli imara,
iii. Kila mwanafunzi aje na vyombo vya chakula yaani sahani moja, bakuli moja, kikombe na kijiko kimoja,
iv. Kutokana na hali ya udongo wa shuleni mwanafunzi anatakiwa kuja na mabuti ya mvua (gunboots).

**4.0. SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE**

**4.1. MAMBO YA KUZINGATIA SHULENI**

i. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya darasa ni muhimu,
ii. Kuwahi katika kila shughuli ya shule atakayopangiwa,
iii. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo shule hii,
iv. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule,
v. Kuvaa sare ya shule wakati wote awapo shuleni na nje ya shule na anapokuwa kwenye shughuli za kitaaluma,
vi. Kuzingatia ratiba ya Shule wakati wote,
vii. Sare za shule huvaliwa wakati wote ukiwa shuleni, wakati wa kwenda nyumbani, na wakati wa kurudi shuleni,
viii. Lugha ya mawasiliano awapo shuleni kwa muda wote ni kiingereza,
ix. Mwanafunzi awe na bidii ya kujielimisha na kufanya mazoezi na majaribio yote darasani na mitihani yote ikiwemo ya nje. Kila mwanafunzi anatakiwa kufaulu wastani wa alama 65%,
x. Kila mwanafunzi atawajibika kulinda na kutunza mali ya shule na yake binafsi, kwa Mwanafunzi atakaye haribu mali ya shule atapaswa kulipa mara moja baada ya kuthibitika,
xi. Kila mwanafunzi analazimika kuwa na nidhamu ya hali ya juu katika Maongezi na walezi wake pasipo kutumia lugha chafu, na
xii. Kutokuwa na chakula cha aina yoyote bwenini.

### 4.2. MAKOSA YA KUWEZA KUKUFUKUZISHA SHULE

i. Wizi,
ii. Kugoma na kuhamasisha mgomo,
iii. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu, au mtu yeyote yule,
iv. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule,
v. Ulevi au unywaji wa pombe, matumizi ya madawa ya kulevya na uvutaji wa sigara,
vi. Uasherati, uhusiano wa kimapenzi jinsia moja, kuoa au kuolewa,
vii. Kushiriki, matendo ya uharifu,siasa na matendo yoyote yanayo vunja sheria za nchi,
viii. Kutembelea majumba ya starehe (Baa, Kumbi za muziki) na nyumba za kulala wageni (Guest House)
ix. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu za mkononi, Laini au kukutwa na chaja ya simu katika mazingira ya shule,
x. Kunyoa mitindo (panki, kiduku, kipara) na kufuga ndevu,
xi. Kudharau bendera ya Taifa,
xii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, kutishia kujiua kama kunywa sumu, na
xiii. Uharibifu wa mali ya umma kwa maksudi.

### 5.0. MAMBO MENGINE MUHIMU.

i. Fomu ya uambatanisho wa afya (medical examination form) ijazwe na Mganga wa Hospitali,
ii. Fomu ya taarifa muhimu ,ijazwe kikamilifu na kusainiwa na mzazi na mwanafunzi,
iii. Fomu ya mkataba wa kutoshiriki migomo fujo na makosa ya jinai, ijazwe na kusainiwa na mzazi na mwanafunzi,

**N:B Tafadhali fomu hizi ziwasilishwe siku ya kuripoti shuleni zikiwa zimeambatishwa na kivuli cha cheti cha kuzaliwa.**

### 6.0. MAWASILIANO.

i. Mkuu wa Shule: 0768078372,
ii. Makamu Mkuu wa Shule: 0698853031.

*MOTO:BEHAPPY,BEENERGETIC,BEYOU,THINKSCHOOL.*
KARIBUSANASHULEYASEKONDARIKAKONKOBOYS.

ROGERSMUTALEMWAKILLO.
**MKUUWASHULE.**

THE HEAD OF SCHOOL
KAKONKO BOYS SECONDARY SCHOOL
P.O Box 03 KAKONKO

**AHADI YA UTII WA SHERIA ZA SHULE, KUTOSHIRIKI MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI**

Mimi ………………………………………………………………………naahidi kufuata sheria na taratibu zote za shule kadri zilivyotolewa na zitakavyotolewa na uongozi wa shule muda wote niwapo shuleni na kwamba sitashiriki migomo, fujo wala makosa yoyote ya jinai. Pia naahidi kuwa nitakuwa mwaminifu kwa uongozi wa shule na jumuiya nzima ya shule ya sekondari ya wavulana Kakonko.

……………………………… … …………………….

Saini ya mwanafunzi Tarehe

………………………………… …………… ……. …………… ………………

Jina la mzazi/mlezi Saini Tarehe

**HISTORIA YA MWANAFUNZI**

1. Jina kamili (kama ilivyo kwenye matokeo ya darasa la saba):
   …………………..………………………………………………………………………
2. Tarehe ya kuzaliwa.........................................................................................
3. Jina la Baba…………………………………………………………………………
4. Jina la Mama……………………………………………………………………….
5. Jina kamili la Mlezi…………………………………………………………………
6. Anuani ya Mzazi/Mlezi…………………………………………………………….
7. Uhusiano wa Mlezi…………………………………………………………………
8. Kazi ya Baba (Mkulima,Mfanyabiashara, Mfanyakazi)……………………………
9. Kama ni Mkulima ni zao gani analolitegemea…………………………………..
10. Kama ni Mfanya Biashara, Biashara yake ni………………………………………
11. Kama ni Mfanyakazi, kazi yake ni………………………………………………...
12. Afya ya Mwanafunzi, kama anayo matatizo ya kiafya na hivyo hustahili huduma maalumu, Tafadhari Mzazi/Mlezi aeleze wazi:
    ……………………………………………………………………………………
    ……………………………………………………………………………………
    ……………………………………………………………………………………
13. Dini yangu ni………………………………………………………………………
14. Ndugu wa karibu:-

i. Jina …………………………………Uhusiano ……..............Simu………….
ii. Jina …………………………………..Uhusiano………………Simu…………...
iii. Jina …………………………………..Uhusiano ………………Simu ………….

| Pasipoti ya i | Pasipoti ya ii | Pasipoti iii |
|---|---|---|

MEDICAL EXAMINATION FORM

Student's names…………………………………………………………………………………

Age……………………………………………………………………………………………..

Stool test……………………………………………………………………………………….

Blood group……………………………………………………………………………………

Urine analysis………………………………………………………………………………….

Syphilis test……………………………………………………………………………………

Chest test………………………………………………………………………………………

Speech test…………………………………………………………………………………….

Eye test………………………………………………………………………………………...

Abdomen test………………………………………………………………………………….

Additional information and physical defect or impairment to pursue further education

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

Name…………………………………………………………………………………………...

Signed…………………………………………………………………………………………

Designation…………………………………………………………………………………….

Official stamp

Date………..